# TABATA WELFARE ASSOCIATION

**Mtaa wa Liwiti, Kata ya Liwiti, S.L.P 21715, Dar es Salaam,**

**Barua pepe: info@tabatawelfare.co.tz**

**Simu: +255 783 249 255 Tovuti: - www.tabatawelfare.co.tz**

***REG. No. 020S.A.2308700871***


## TANGAZO RASMI LA UCHAGUZI KWA WANACHAMA WA TWA

Yah: **RIPOTI YA MAENDELEO YA TWA KWA KIPINDI CHA UONGOZI WA MPITO NA UCHAGUZI WA VIONGOZI**

**Ndugu Wanachama wa Tabata Welfare Association (TWA),**

1. Kama mnavyofahamu, mnamo tarehe **10 Novemba 2024**, kupitia **Mkutano Mkuu wa Wanachama** uliofanyika siku ya Jumapili tarehe 10/11/2024 katika Ukumbi wa Nderingo, Tabata – Dar es Salaam, Umoja wetu ulifanya mabadiliko ya kiutawala na kuchagua **Uongozi wa Mpito**. Hatua hiyo ililenga kurejesha utulivu, kuimarisha mshikamano, na kuboresha mifumo ya uendeshaji chama

2. Uongozi wa Mpito unapenda kuwafahamisha rasmi wanachama wote kuwa sasa tumeingia katika hatua ya mwisho ya mchakato wa mpito, kuelekea kupatikana kwa uongozi mpya wa kudumu wa Tabata Welfare Association (TWA) kupitia mchakato wa uchaguzi ulio huru na wa haki.

3. Kwa msingi huo, Uongozi wa Mpito unawataarifu rasmi wanachama ratiba ya mikutano miwili muhimu itakayowezesha kukamilisha mchakato huu wa kihistoria kwa Umoja wetu kama ifuatavyo:

### *1.* MKUTANO WA KUCHAGUA KAMATI YA UCHAGUZI K*wa njia ya Whatsapp)*

***a) Hatua ya Kwanza:*** *Kuchukua Fomu za Kugombea*

Mara tu baada ya kutolewa kwa tangazo hili rasmi, wanachama wote wenye nia ya kugombea na wanaokidhi vigezo vya kikatiba na kikanuni wanaruhusiwa kuchukua fomu za kugombea nafasi husika.

**Utaratibu wa kuchukua fomu ni kama ifuatavyo:**

1. Mwanachama aliyeonyesha nia ya kugombea na anayestahili atawasiliana na Uongozi wa Mpito kupitia njia zilizotangazwa ili kupatiwa fomu ya kugombea.
2. Fomu za kugombea zitatolewa kwa wanachama wanaostahili pekee, baada ya kuthibitishwa kwa sifa zao kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Umoja.
3. Endapo mwanachama atakumbana na changamoto yoyote katika mchakato wa kuchukua au kujaza fomu, anaruhusiwa kuwasiliana na Uongozi wa Mpito kwa maelezo zaidi.

***b) Hatua ya Pili:*** *Kurejesha Fomu za Kugombea*

- **Tarehe:** 23 Januari 2026
- **Muda:** Saa 2:00 Asubuhi – 10:00 Jioni
- **Jukwaa:** Inbox (WhatsApp) ya Mwenyekiti na, au Katibu wa Uongozi wa Mpito.

**Ajenda Kuu:**

- Kupokea fomu zote zilizojazwa kutoka kwa wanachama wanaogombea nafasi katika Kamati ya Uchaguzi.

Wanachama wote waliochukua na kujaza fomu hizi, wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanazirejesha kwa Mwenyekiti na, au kwa Katibu wa Uongozi wa Mpito, ndani ya muda uliotajwa hapo juu. Fomu zitakazowasilishwa nje ya muda hazitapokelewa.

***c) Hatua ya Tatu:*** *Kutangazwa kwa Majina ya Wagombea*

- **Tarehe:** 24 Januari 2026
- **Muda:** Saa 11:00 Jioni
- **Jukwaa:** Group rasmi la WhatsApp la TWA

**Ajenda Kuu:**

1. Uongozi wa Mpito kutangaza rasmi majina ya wanachama wote waliorejesha fomu za kugombea.

2. Kuwajulisha wanachama orodha kamili ya wagombea watakaoshiriki katika uchaguzi wa Kamati ya Uchaguzi.

***d) Hatua ya Nne:*** *Uchaguzi wa Kamati ya Uchaguzi*

- **Tarehe:** 25 Januari 2026
- **Muda:** Saa 2:00 Asubuhi – 12:00 Jioni
- **Jukwaa:** Group rasmi la WhatsApp la TWA

**Ajenda Kuu:**

1. Kufanya uchaguzi wa Kamati ya Uchaguzi yenye muundo ufuatao:

    - Mwenyekiti – 1
    - Katibu – 1
    - Wajumbe – 4

Kamati hii itakuwa na jukumu la kusimamia mchakato mzima wa Uchaguzi Mkuu wa viongozi wa TWA kwa uwazi, uadilifu, na kwa kuzingatia Katiba na Kanuni za Umoja.

## 2. MKUTANO MKUU WA WANACHAMA NA UCHAGUZI MKUU

Baada ya kuundwa rasmi kwa Kamati ya Uchaguzi, Uongozi wa Mpito utaitisha Mkutano Mkuu wa Wanachama wote, ambao utakuwa hatua ya mwisho ya kukamilisha mchakato wa mpito na kuwapata viongozi wapya wa Tabata Welfare Association (TWA).

**Taarifa za Mkutano Mkuu:**

- **Tarehe:** 8 Februari 2026
- **Mahali:** Patatangazwa rasmi na Kamati ya Uchaguzi.

**Ajenda Kuu za Mkutano Mkuu:**

**1. Uongozi wa Mpito kutoa Taarifa Kamili ya Maendeleo (Progress Report):**

- Hali ya Umoja kabla ya Uongozi wa Mpito
- Majukumu yaliyotekelezwa katika kipindi cha mpito
- Hatua zilizochukuliwa kurejesha utulivu na mshikamano
- Changamoto zilizojitokeza
- Hali ya jumla ya uendeshaji wa Umoja kwa sasa
- Mapendekezo na ushauri kwa uongozi mpya

**2. Kamati ya Uchaguzi kusimamia Uchaguzi Mkuu wa Viongozi wa TWA:**

- Kupokea wagombea waliothibitishwa
- Kuendesha zoezi la upigaji kura kwa uwazi na haki
- Kuhakikisha taratibu zote za uchaguzi zinafuatwa kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za TWA

**3. Kutangazwa kwa Matokeo ya Uchaguzi na Makabidhiano Rasmi:**

- Kutangaza viongozi wapya waliochaguliwa
- Kufanyika kwa makabidhiano rasmi kati ya Uongozi wa Mpito na Uongozi Mpya
- Kufungua ukurasa mpya wa uongozi na maendeleo ya TWA

4. Mkutano huu wa **tarehe 8 Februari 2026** utakuwa chini ya usimamizi kamili wa Kamati ya Uchaguzi itakayochaguliwa **tarehe 25 Januari 2026**. Hivyo, maamuzi yote yatakayofikiwa siku hiyo yatakuwa na uhalali kamili wa kikatiba na ridhaa ya wanachama.

5. Uongozi wa Mpito unaamini kuwa mkutano huu utakuwa fursa muhimu ya kuimarisha demokrasia ndani ya TWA, kurejesha mshikamano, na kujenga misingi imara ya maendeleo endelevu ya Umoja wetu.

6. Hivyo basi, Uongozi wa Mpito unatoa wito maalum kwa wanachama wote kushiriki kikamilifu katika mikutano hii miwili muhimu. Huu ni wakati wa kihistoria kwa Umoja wetu, na mafanikio ya mchakato huu yanategemea umoja, ushirikiano na uwajibikaji wa kila mwanachama.

Tushirikiane kwa moyo mmoja kuhakikisha TWA inapata uongozi mpya ulio imara, halali na wenye ridhaa ya wanachama wote.

**TWA, PAMOJA TUNAWEZA, PAMOJA TUNAFANIKIWA!**

***Imetolewa na:***
**Uongozi wa Mpito**
**Tabata Welfare Association (TWA)**
**Tarehe: 21/01/2026**